# LEARNING BY EAR

# "If a tree falls… - Deforestation in Africa"

## EPISODE TWO: "Macro vs. Micro Solutions"

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

**List of characters EPISODE TWO:**

**Narrator**

**SCENE 1 Mulogo (m, 22)**

**SCENE 2 Chief Apaloo (m, 40) Mulogo (m, 22)**

**SCENE 3 Chika (f, 18) Talib (m, 20)**

**SCENE 4 Mulogo (m, 22) Isi (m, 18)**

**SCENE 5 Mother (f, 36) Akiki (f, 7)**

**SCENE 6 Chika (f, 18) Isi (m, 18)**

## INTRO

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na kipindi cha pili cha mchezo wetu mpya wa redio kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinasimuliwa kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajipata pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Kufikia sasa, vijana walioko katika kambi ya Dovani wamejifunza jinsi mvua inavyotokea. Lakini wanawezaje kutatua tatizo la upungufu wa kuni na maji kambini? Isingoma na Mulogo, ambao ni watoto wa machifu, wanabishana kuhusu ufumbuzi wa matatizo kwa siku za usoni kama walivyokuwa wakifanya baba zao nyumbani. Jiunge nasi tumsikie Mulogo mwenye umri wa miaka 22 akilalamikia hali ya watu kutochangamkia teknolojia ya kisasa kutanzua matatizo makubwa.

### Episode TWO: <u>“Macro v. Micro Solutions.”</u>

**1.MUSIC UP**

**Scene 1**

**2.MULOGO NARRATOR: (irritated voice)** Jina langu ni Mulogo. Nina umri wa miaka 22 na ninatosha kupiga kura, kuoa lakini jamaa wananitendea kama kwamba mimi ni punguani! Nina fikra nyingi za maana lakini hakuna anayenizingatia. Nimekwamilia hapa katika kambi ya Dovani sasa imetimu miezi sita. Hakuna jengine ninalopata ila wazo la Talib na Chika kwamba tung’oe magugu na tupande maharagwe aina ya soya. Hivi hawa jamaa wanataka tuishi maskini wa daima? Babangu ni Chifu Apaloo. Jana usiku tuligombana kuhusiana na jamii yetu katika wilaya ya Abanto, tulipokuwa tukiishi kabla ya vita kusababisha tukimbilie huku. Eneo lenyewe lina misitu mingi ya nyanda za juu. Tunapoteza pato kuu ambalo tungepata lau tungewaruhusu wakataji mbao kama babake Isi alivyofanya. Chifu Kipko alikuwa mtu wa maendeleo. Alijua kwamba tulihitaji mbao- maanake mbao- za kujenga nyumba, fanicha, nyua.... na tunaweza kuuza mbao zenyewe kote ulimwenguni- Uchina..Ulaya....

Wanazitaka mbao zetu. Lakini mzee hakutaka kusikiliza wazo langu zuri …

**3. MUSIC TO INDICATE FLASHBACK. HOLD UNDER**

**Scene 2**

**4. SFX Night sounds**

**5.APALOO:** Ninakusikiliza mwanangu, lakini pia niliwasikiliza watu wazima wanaokumbuka wakati tulipokuwa na kila kitu – ardhi, misitu, wanyamapori, mashamba na maji. Kuna mambo mawili unayoyasahau- mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la idadi ya watu. Maisha yetu yanategemea misitu hiyo na madimbwi hayo. Idadi yetu watu wa Abanto imeongezeka mara mbili na misitu na madimbwi yetu karibu yote yametoweka. Chifu Kipko alifanya kosa kubwa kuruhusu upandaji wa miti ya kukatwa mbao. Hatua hiyo ilisababisha watu wengi wapya kuja katika eneo letu wakitafuta kazi, wakihitaji ardhi na maji walipokuwa wakikata misitu yetu.

**6.MULOGO:** Chifu Kipko alikuwa na wazo zuri! Baba! Tunaweza kujipatia dola milioni moja za Marekani na kwa fedha hizo tunaweza kujenga barabara, hospitali, shule, na mfumo mzuri wa kuzoa maji taka. Kazi zote hizo zinahitaji fedha nyingi. Hatuwezi kupata fedha za kutosha kwa kuuza mafuta ya alizeti katika soko la Abanto. Kwa hisani yako! Tafadhali zingatia ninayosema!

**7.APALOO:** Chifu Kipko alisababisha mgogoro na kutuletea ardhi kame. Kwani hukumbuki? Umesahau?

**8.MUSIC UP**

**Scene 3**

**9. SFX Daytime. Interior office / fax machine and paper**

**10.CHIKA:** Talib! Habari za hivi punde zinasema kuwa kumekuwa na maporomoko ya ardhi katika Mlima Elgon. Watu zaidi ya mia tatu wamefariki dunia.

**11.TALIB:** Ati? Ni kiasi miezi miwili hivi tangu walipotangaza kuhusu ukame ambao haujawahi kupatikana kwa muda wa miaka hamsini. Kwani kuna nini?

**12.CHIKA: (Reading slowly)**

“Joseph Muyera, afisa wa kundi la jamii la kuhifadhi mazingira katika wilaya ya Manafwa amesema: Idadi kubwa ya watu katika eneo la Mlima Elgon imetatiza hali ya mazingira ya eneo hilo. Mazingira yetu yanaharibiwa kwa kasi kubwa; watu wanakata miti kwenye mlima, wakiingilia chemchemi za maji, ‘ alisema. ‘Theluji iliyopo juu ya Mlima Elgon inayeyuka.’”

**13.TALIB:** Chika! Hatari hiyo!

**14.CHIKA:** Theluji hiyo ikiyeyuka kabisa wakulima wote walio kwenye bonde watakosa chanzo chao kikuu cha maji.

**15.TALIB:** Hii ndiyo dalili halisi ya mabadiliko ya hali ya hewa. Yaani- hali ya hewa katika bara letu ni tofauti na kwengine lakini wakulima wanasema mambo yamebadilika zaidi miaka ya hivi karibuni. Watu mia tatu wanaangamia vivi hivi – pamoja na mimea yao yote ya mazao.

**16.CHIKA:** Miche 1,500 ya miti imesombwa, na inasemekana hapa, mvua kubwa imenyesha kwa hiyo siku moja. Hebu fikiria Talib – maji yote hayo. Yamepotea bure.

**17.TALIB:** Bila misitu ya kukinga udongo wa juu, mimea na miche nayo pia huharibiwa. Haiwezi kuhimili hali. Samahani Chika. Wakati unatutupa mkono.

**<u>18.MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 4</u>**

**<u>19. SFX Daytime ambience outside</u>**

**20.MULOGO:** Wayaonaje macho ya Chika? Yanapendeza? Hasa jicho lake la kulia. Linapendeza ajabu!

**21.ISI:** Sijawahi kumkaribia kiasi cha kutazama macho yake.

**22.MULOGO: (Laughing)** Nimemkaribia!

**23.ISI: (very seriously)** Je, Mulogo, uliondokewa na jamaa yako yeyote kwenye vita?

**24. MULOGO: (stops laughing)** Hapana. Sisi tulibahatika. Sote tulinusurika. Mbona unaniuliza hivyo?

**25.ISI:** Naam…Nina mambo mengine yanayonishughulisha akilini mwangu kuliko hayo ya kutazama macho ya msichana. Labda ndugu yangu Jamal anateswa sasa hivi. Na baba yangu. Na ndugu yangu pacha Kato...

**26.MULOGO:** Samahani! Pole! Pole sana Isi. Bila shaka. Lakini... hata hivyo... mwanamke mrembo anaweza kukutuliza akili. Anatoka wilayani kwetu na nikwambie jambo?

**27.ISI: (not interested)** Nini?

**28.MULOGO: (proudly)** Siku moja …atakuwa…. Mke wangu!

**29.ISI:** Unajuwaje! Unajiamini sana wewe!

**30.MULOGO: (laughing)** Bila shaka! Mimi ni mwana wa chifu! Na wewe pia!

**31.ISI: (sarcastic)** Asante Mulogo kwa kunikumbusha! Haya! Unataka kunionyesha nini?

**32.MULOGO:** Tazama hapa!

**33. SFX Paper noise - Unrolling a chart**

**34.MULOGO:** Tunataka kuacha kutegemea kuni kupikia, sivyo?

**35.ISI:** Ndivyo! Lakini vipi?

**36.MULOGO:** Tunahitaji nguvu za umeme na tunaweza kuzipata kwa nishati ya jua au upepo …..**(whispering)** maji! Tazama! Kilomita thelathini kaskazini mwa Wilaya ya Abanto kuna maporomoko ya maji ya Talari. Maji yanayopatikana wakati wa mvua ni mengi sana na yanapiga kwa nguvu – hebu fikiri hiyo nguvu – hebu kisia nishati iliyopo. Na hapa.. tazama..hapa kuna mkono wa mto na pia ziwa upande wa chini wa maporomoko. Kwa hivyo hilo ndilo eneo lifaalo kujenga bwawa kubwa la maji. Maji yatakingwa hapo na tunaweza kuyatumia kunywa na pia kunyunyuizia mashamba. Nguvu za maji ya maporomoko zina uwezo wa kusukuma mitambo itakayoendesha majenereta. Waona? Tunaweza kupata nguvu za umeme za bei nafuu kwa eneo lote.

**37.ISI:** Mpango mzuri. Sasa nimefahamu unalosema unaposema tunatakiwa kuwa na fikra pevu kuliko kuzungumza juu ya kuokoa madimbwi yetu!

**38.MULOGO:** Ndo hivyo. Na mimi na wewe tunaweza kushirikiana kutekeleza mradi huo!

**39.ISI:** Ati? Mulogo, una maana gani?

**40.MULOGO:** Ninasema kwamba, sisi ni vijana na akili zetu. Hatutaishi kwenye kambi hii maisha yetu yote. Vita vitakwisha na itatubidi kurejea wilayani kwetu. Sisi ndio mustakabali wa eneo letu, Isi. Tunapaswa kushirikiana.

**41.ISI:** Unatafuta mtu wa kuwa na ubia nawe. Kwa nini mimi?

**42.MULOGO:** Wewe ni mwana wa chifu. Na mimi pia ni mwana wa chifu.

**43.ISI:** Umeshaniambia hilo tayari!

**44.MULOGO:** Sisi tumezaliwa katika mazingira ya uongozi. Tunapaswa kuiongoza nchi yetu kuelekea mustakabali wake.

**45.ISI:** Kwa hali hiyo tunatakikana kuangaza mbele.

**46.MULOGO:** Na ndivyo ninavyojitahidi kufanya.

**47.ISI: (Sarcastic)** Lakini bado! Kuna mambo madogo madogo ambayo huzingatii... mabadiliko ya hali ya hewa, ongezeko la joto duniani, ongezeko la idadi ya watu, kupungua rasilimali zetu.

**48.MULOGO:** Ndivyo ninavyosema! Ufumbuzi wa kina kwa matatizo sugu!

**49.ISI:** Nisikilize. Kitambo kidogo nilisikiliza kipindi fulani kwenye redio …kuhusu Ziwa Chad nchini Naijeria, kuna wakati lilikuwa mojawapo ya maziwa makubwa duniani. Ziwa hilo limepoteza asilimia 90 ya maji yake na linaelekea kutoweka – kwa nini? Mvua chache, uharibifu wa misitu na mradi wako huo wa utoaji wa nguvu za umeme, yote hayo yanamaliza maji ya ziwa hilo. Watu milioni thelathini wataachwa bila chanzo muhimu cha maji. Usisahau ukosefu wa samaki na watu kutatizika maisha yao. Unataka niendelee kukupasha?

**50.MULOGO: (unsure of himself)** Ehe! Labda. Kweli. Lakini unakubaliana nami tunapaswa kuanza kuzingatia mambo, Isi! Tafadhali! Usiwe mtu wa kukata tama upesi.

**51.MUSIC UP**

**Scene 5**

**52. SFX Night sounds / inside**

**53.MOTHER:** Akiki njoo**.** Kunywa maziwa kidogo kidogo na mimi nitakusimulia hadithi nzuri sana leo usiku.

**54.AKIKI: (Sips loudly)** Nimeyamaliza yote. Ma, naweza kulala katika kitanda chako?

**55.MOTHER: (Softly)** Unaweza. Sasa, ebu nikusimulie hadithi ya jinsi mti ulivyomuokoa mwanamume fulani mzee.

**56.AKIKI: (sleepily)** Haya ma.

**<u>57.FADE IN AFRICAN DRUM SOUNDS. HOLD UNDER</u>**

**58.MOTHER:** Wajua Akiki, ngoma kubwa tunayopigia muziki inatengenezwa kutokana na aina fulani ya mti wa mbuyu. Mti huo unapatikana ndani kabisa ya misitu ya Afrika Mashariki na kwa mamia ya miaka watu wetu wamekuwa wakiutumia kutengeneza ngoma zao. Mti huo unasemekana kwamba una sauti nzuri na una sifa za kiroho. Basi siku moja mzee mmoja alikwenda kutafuta mahali pa kujificha kutokana na watu waovu waliokuwa wakikata miti na kuvichoma vijiji. Akaupata mti huo. Kulikuwa na baridi. Mzee akawasha moto ili aote. Lakini mvua kubwa ilikuwa ikinyesha pamoja na upepo mkali.

**(same sound bite)MOTHER (contd):** Mvua ikasema,, "Nitakuonyesha mahali pakavu." Mzee akauliza, "Mahali gani pakavu?" Mvua ikasema, "Ingia ndani ya mbuyu"...

**<u>Slowly fade out both music and mother</u>**

**(same sound bite) MOTHER:** …Mzee aliingia ndani ya mti huo. Ndani kulikuwa kukavu. Akaihisi roho ya mti. Alilala fofofo na akaota kwamba alisikia sauti tamu ya ngoma ikipigwa na ikimlinda.

**Scene 6**

**59. SFX Night sounds Footsteps on sand/gravel approaching**

**60. Isi is humming a sad song**

**61.CHIKA:** **(from some distance**) Isi? Upo?

**62.ISI:** Nani. Nani mwenzangu?

**63.CHIKA:** **(closer)** Ni mimi, Chika! Nimekuja kukwambia... kuna watu 60 kutoka Wilaya ya Abanto watakaoletwa kwa lori juma lijalo. Utaweza kunisaidia kuwasajili wote?

**64.ISI: (breathless)** Chika? Unafikiri? Inawezekana…?

**65.CHIKA:** Najua una hamu sana Isi kujua mambo yalivyo. Tusubiri tuone vile itakavyokuwa. Alamsiki.

**66. SFX: FOOTSTEPS DEPARTING (FADE)**

**67.ISI: (whispering)** Kwa hisani yako Kato...Kwa hisani yako uwe miongoni mwa wataoletwa kwa lori!

**68. MUSIC UP**

**OUTRO.**

Na huo kwa leo ndio mwisho kipindi chetu cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* cha mchezo wa redio “Mti unapoanguka...” ulioandikwa na Romie Singh na unaoshughulikia suala la uharibifu wa misitu. Wanawake ndiyo watumizi sana wa misitu na kwa hivyo wanatakikana kuhusishwa kusimamia matumizi ya kuni katika jamii zao na pia kutafuta njia mpya za kuokoa miti. Tafadhali jiunge nasi tena kwenye kipindi cha tatu. Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwa heri kwa sasa.

**END OF EPISODE TWO**